

SOUTH EAST JUNIOR HIGH

(SHULE YA UPILI YA VIJANA YA KUSUNI MASHARIKI)

Dr. Amber Boyd, Mkurugenzi

Michelle Cook, Msaidizi wa Mkurugenzi

2501 Bradford Drive
Iowa City, IA 52240
Simu (319) 688 -1070
Faksi (319) 688 -1079

Januari, 2016

Kwa Wazazi/Walezi wa wanafunzi wa darasa la saba wa mwaka wa 2016-2017 katika shule ya upili ya vijana ya Kusini Mashariki (South East Junior High)

Karibuni katika shule ya South East Junior High! Tunatazamia kufanya kazi na wewe na mtoto wako. Katika wakati huu tunaongea na mtoto wako na tunataka kujua maoni yako kuhusu mwenendo wa mpangilio wa masomo mtoto wako anapojiandikisha katika masomo ya mwaka wa 2016-17. Ili kusaidia katika mwenendo huu, wasimamizi wa shule na waongozi wa mashauri katika shule ya South East wangependa kuwaelezea kuhusu tarehe za mwisho na miongozo ambayo itatusaidia kukusanya habari na kujenga mpangilio wa masomo ambao utakidhi mahitaji wa wanafunzi.

Jumatano, Januari 27, 2016 6:30 PM (JIONI)

Mkutano wa wazazi wa wanafunzi wa darasa la sita (6th) utakuwa katika shule ya South East Kafeteria/Chumba Kikubwa katika ghorofa ya chini

Ijumaa, Januari 29, 2016

Siku ya mwisho ya wanafunzi wa darasa la sita (6th) kurudisha fomu ya kujiandikisha kwa mwalimu wao wa homeroom.

Kama mtoto wako anataka kuchukua somo la kujichagulia, tafadhali andikisha somo hilo sasa. Maadamu wanafunzi wa kutosha wanajiandikisha kuchukua somo hilo, tutajaribu kuliweka kwenye mpangilio. Juhudi zetu katika majira hii ya joto zitakuwa kujenga mpangilio wa masomo kulingana na maombi yenu na kusawazisha ukubwa wa madarasa ma matayarisho ya waalimu katika mwaka mzima wa shule. Kwa hivyo, maombi yafuatayo PEKEE ndiyo tu yatafikiriwa katika muhula wa fall (na yatafikiriwa tu katika siku tatu za kwanza za trimester).

- Kubadilisha kati ya kila-siku-ingine ya Study Hall na PE ili kusawazisha idadi ya study halls katika siku moja (Kumbuka: Wasimamizi hawawezi kuzidisha mipaka ya idadi ya darasa ili kukamilisha badiliko hili.)
- Kuachilia somo ambalo halihitajiki ili kusonga mbele.
- Kuongeza somo katika darasa ambalo lina nafasi iliyoachwa na mwanafunzi mwingine ama katika study hall (Kumbuka: Wasimamizi hawawezi kuzidisha mipaka ya idadi ya darasa ama kubadilisha mapangilio wa masomo ili kukamilisha badiliko hili.)

Mwalimu wa mtoto wako wa darasa la sita (6th) atakuwa ameamua darasa la hesabu ambalo mtoto wako ataandikishwa. Pendekezo la hesabu litaandikwa kwenye fomu ya kujiandikisha ya SEJHS pamoja na masomo mengine yote yaliyochaguliwa. Ikiwa unataka rufaa ya uamuzi huu, tafadhali fuata utaratibu ulioandikwa nyuma ya fomu ya hesabu.

Lengo letu katika South East ni kumpatia mtoto wako nafasi bora ya elimu na uchunguzi. Kila siku kwa siku, hii inamaanisha kuwa wafanyikazi na wasimamizi wa South East wanajitahidi kukidhi mahitaji na kutimiza maombi ya mtu binafsi ya wanafunzi 800 huku wakidumisha elimu yetu ya kiwango cha juu na wakifanya kazi ndani ya rasimali zetu zilizotengwa. Tunakukaribisha kuwa mshirika katika kutekeleza lengo hili na tunashukuru kwa msaada wako..

Wako Mwaminifu,

Dr. Boyd
Mkurugenzi wa Shule ya South East Junior High